**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA RAIS**

**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

# MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE ZA SEKONDARI ZA SERIKALI TANZANIA

**Juni, 2023**

**Dodoma**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**OFISI YA RAIS – TAMISEMI**


**Namba za Simu:**

**Mkuu wa Shule: 0762738564**
**Makamu Mkuu wa Shule: 0764921641**
**Matron: 0742015295**
**Shule ya Sekondari Udzungwa**
**S.L.P. 1693**
**NAMBA YA USAJILI NECTA: S**

**Tarehe 12/06/2023**

**Mzazi/Mlezi wa Mwanafunzi ………….**
**……………………………………………..**
**S.L.P ……………………………………..**
**…………………………………………….**

**Yah: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE YA SEKONDARI UDZUNGWA HALMASHAURI YA KILOLO MKOA IRINGA MWAKA 2023**

**1.** Nafurahi kukutaarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na Kidato cha Tano katika Shule hii mwaka 2023 na atasoma tahasusi ya …….……

Shule ya Sekondari Udzungwa ipo umbali wa Kilometa 58 Kusini Mashariki mwa Mji wa Iringa. Usafiri wa basi kutoka mjini Iringa unapatikana katika kituo cha mabasi Mlandege. Nauli ni Shilingi 4,000/=.

Muhula wa Masomo unaanza tarehe 14 Agosti, 2023. Hivyo mwanafunzi anatakiwa kuripoti shuleni tarehe 13 Agosti, 2023. Mwisho wa kuripoti ni tarehe 31 Agosti, 2023.

## 2. Mambo muhimu ya kuzingatia:-

### 2.1 Sare za Shule

i. Sare ya shule hii ni sketi za rangi ya bluu bahari mbili, ndefu zinazovuka magoti zenye marinda nane.Suruali mbili pana rangi ya sketi,nusu kanzu mbili zinazofika kwenye magoti. Hizi ni kwa waislaumu tu.
ii. Mashati meupe ya mikono mirefu mawili.
iii. Rangi ya Hijab (kijuba) ni nyeupe ifunike kifua cha mwanafunzi pia iwe ndefu kufikia kifundo cha mkono akisimama.
iv. Sare ya Michezo ni track suit nyekundu jozi mbili.
v. Viatu vya shule ni vyeusi vya kufunga na kamba vyenye visigino vifupi;
vi. Soksi jozi mbili nyeupe.
vii. Sweta rangi ya maziwa (cream) jozi mbili mikono mirefu.
viii. Nguo za kushindia (*shamba dress*) ni rangi ya dark blue mbili, ndefu zinazovuka magoti zenye marinda nane.
ix. Tai ndefu rangi ya bluu bahari.
x. Tisheti (T-shirt) moja rangi ya kijivu yenye kora (form six).

### 2.2 Mahitaji mengine muhimu ambayo mwanafunzi anapaswa kuja nayo shuleni:-

i. Madaftari kumi(counter books quire 4).
ii. **Ream (A4)** ya Karatasi Mbili (2) kwa mwaka;
iii. Vitabu vya masomo ya tahasusi husika.
iv. Dissecting Kit kwa wanafunzi wanaosoma Biology;
v. Scientific Calculator;
vi. Godoro 3x6 inchi 5 unene.
vii. Mashuka Jozi 2 rangi ya pink, blanket 1, foronya ya godoro 1, chandarua 1 rangi nyeupe.
viii. Nguo za ndani za kutosha;
ix. Vyombo vya chakula (sahani, bakuli, kijiko na kikombe);
x. Ndoo 2 ndogo (lita Kumi) zenye mifuniko;
xi. Kwanja 1, jembe 1, reki 1, mifagio 2 wa ndani na nje.

### 2.3 Michango mbalimbali

| Na | Aina ya Mchango | Kiasi |
|---|---|---|
| 1. | Mchango wa Uendeshaji wa Shule | 65,000/= |
| 3. | Tahadhari | 5,000/= |
| 4. | Nembo | 5,000/= |
| 5. | Kitambulisho cha Shule | 5,000/= |
| | **Jumla** | **80,000/=** |

**Michango yote ilipwe kupitia akaunt namba 62302300243 NMB, Jina la akaunt Elimu ya Kujitegemea Shule ya Sekondari Udzungwa**

## 3. Sheria na Kanuni muhimu za Shule

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyo rekebishwa kwa Sheria Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha, inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia yenye dhamana ya elimu na Ofisi ya Rais – TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji wa elimu nchini. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yanafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni. Mambo hayo ni pamoja na;

### 3.1 Sheria na Kanuni za Shule

i. Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.;
ii. Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule;
iii. Kushiriki kwa kikamilifu masomo ya usiku( Preparation);
iv. Kuwahi katika kila shughuli za shule utakazopewa;
v. Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo ya kuwepo ndani na nje ya shule ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii;
vi. Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule;
vii. Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa;
viii. Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote;
ix. Kutunza mali za shule;
x. Ni marufuku mwanafunzi kumiliki vifaa vyenye ncha kali na dawa bila idhini ya daktari; na
xi. Mwanafunzi haruhusiwi kubadili dini wala kumshawishi mwanafunzi mwenzake kubadili dini wawapo shuleni.

**MUHIMU:**

- Mwanafunzi hapaswi kuja na simu shuleni kwa namna yoyote ile, na hakuna mtumishi anayeruhusiwa kutunza simu ya mwanafunzi;

- Mwanafunzi awapo shuleni atatakiwa kulala kwenye Bweni alilopangiwa na kitanda alichopangiwa. Ni marufuku mwanafunzi kulala kitanda kimoja na mwenzake au kuishi kwenye Bweni ambalo hakupangiwa. Kitanda kimoja kitatumika na mwanafunzi mmoja tu;

- Mwanafunzi ataruhusiwa kurudi nyumbani kwa ruhusa na kibali maalum toka kwa Mkuu wa Shule. (Msiba au Ugonjwa).

**3.2 Makosa yatakayosababisha Mwanafunzi kufukuzwa Shule ni pamoja na:**

i. Wizi;
ii. Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa/utoro;
iii. Kugoma na kuhamasisha mgomo;
iv. Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu/walezi na jamii kwa ujumla;
v. Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi, kumpiga mwalimu au mtu yeyote yule;
vi. Kusuka nywele kwa mtindo usiokubalika. Wanafunzi wote wanatakiwa kuwa na nywele fupi wakati wote wawapo shuleni au kusuka kwa mtindo wa ususi uliokubalika na uongozi wa shule;
vii. Ulevi au unywaji wa pombe na matumizi ya dawa za kulevya;
viii. Uvutaji wa sigara;
ix. Uasherati, mahusiano ya jinsi moja, kuoa au kuolewa;
x. Kupata ujauzito au kutoa mimba
xi. Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi;
xii. Kwenda kwenye nyumba za starehe na nyumba za kulala wageni;
xiii. Kumiliki, kukutwa au kutumia simu ya mkononi katika mazingira ya shule;
xiv. Kudharau Bendera ya Taifa;
xv. Kufanya jaribio lolote la kujiua, au kutishia kujiua kama kunywa sumu; na
xvi. Uharibifu wa mali ya umma kwa makusudi.

4. **Viambatisho na Fomu Muhimu**

I. **MEDICAL EXAMINATION FORM**

To the medical incharge of ………………………Government hospital. Please examine the above named student as to his/he fitness for further studies.

Name …………………………………………………………….

Blood count (red and white) ………………………………………..

Urine examination …………………………………………………

Stool examination ………………………………………………..

Syphilis test ……………………………………………………

T.B test ………………………………………………………..

Eye test ……………………………………………………………

Ear test ……………………………………………………………….

Spleen test ………………………………………………………..

Abdomen …………………………………………………………

Additional information of any other physical, mental,hereditary or infectious disease.

……………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………..

(Please state nature of treatment)

**MEDICAL CERTIFICATE:**

Icertify that the above mentioned girl/boy has been examined and found fit/not fit to pursue A- level studies.

Signature ………………………………………………..

Designation ………………………………………………

Station ……………………………………………………..

Date ……………………………………………………………

**II. HABARI ZA MWANAFUNZI**

1. Jina kamili (kama ilivyo kwenye vyeti vya mtihani) ……………………………………………………………………….
2. Tarehe ya kuzaliwa………………………………………………
3. Dini……………………………………………………………….
4. Mahali na Wilaya aliyozaliwa ……………………………………………
5. Shule aliyomaliza kidato cha nne …………………………………………..
6. Kazi yoyote aliyowahi kuifanya kama vile kiongozi wa michezo, kwaya, ngoma, kiranja n.k.
7. Mambo anayopendeleya kufanya nje ya masomo (kama michezo, ushonaji n.k)

Ninathibitisha kwamba habari zilizotolewa ni kweli na sahihi.

Jina la mwanafunzi ……………..................... sahihi …………… tarehe……........

**III. HABARI ZA MZAZI / MLEZI**

1. Jina kamili la Baba ………………………….. yupo hai / amefariki.
2. Kazi yake ……………………………………………………………
3. Jina kamili la Mama …………………………… yupo hai/ amefariki.
4. Kazi yake ………………………………………………………….
5. Jina kamili la mlezi (iwapo mtoto haishi na wazazi wake) ………………………………………………………………….
6. Kazi yake …………………………………………………
7. Namba ya simu ya mzazi / mlezi ……………………………..
8. Anuani ya mzazi /mlezi ……………………………………….
9. Mototo anaishi na Baba/Mama/wazazi wote/mlezi (kata lisilohusika).
10. Taja ndugu wanne wa karibu wanaoruhusiwa kumtembelea mwanafunzi awapo shuleni:

| NA | JINA | NA. SIMU | UHUSIANO |
|---|---|---|---|
| 1 | | | |
| 2 | | | |
| 3 | | | |
| 4 | | | |

IV. Picha nne (4) za wazazi na ndugu wa karibu wa mwanafunzi wanaoweza kumtembelea mwanafunzi shuleni.

**5.** Tafadhali soma kwa makini maelezo/maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.

**KARIBU SANA KATIKA SHULE HII**

**Saini ya Mkuu wa Shule ………………**

**Jina la Mkuu wa Shule Asheri M. Manyama**

**Mhuri wa Mkuu wa Shule**

**NB: Kwa siku za hivi karibuni kumekuwa na utapeli (wizi kwa njia ya mitandao). Baadhi ya wazazi wamekuwa wakitumiwa ujumbe mfupi au kupigiwa simu na watu wanaojitambulisha kama walimu na kuwafahamisha kuwa mtoto wa mzazi husika ambaye ni mwanafunzi ni mgojwa na yuko mahututi hivyo mzazi atume pesa. TAFADHALI UPATAPO UJUMBE WOWOTE KUHUSU MWANAFUNZI/MTOTO WAKO USITUME CHOCHOTE, NI VEMA UKAWASILIANA NA UONGOZI WA SHULE KUPATA UKWELI WA TAARIFA HUSIKA KWA NAMBA ZIFUATAZO: -**

- **Mkuu wa shule 0762738564**
- **Makamu Mkuu wa Shule 0764921641**
- **Mwandamizi Taaluma 0756855301**
- **Mwandamizi Malezi 0783641267**